

Magaidi wa MNR wasambaratishwa

Uhuru 20/1/88 p.1 Lead story



NDUGU DAUTO... "Magaidi wajisalimisha."

MAGAIIDI wa MNR wanaosaidiwa na utawala dhalimu wa Makaburu wa Afrika Kusini hawashikili sehemu yoyote ya Msumbiji na hivi sasa wanasambaratika, Waziri wa Sheria wa nchi hiyo, Ndugu Ussumane Ally Dauto alisema jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwa Balozi wa Msumbiji, Ndugu Dauto alisema hivi sasa magaidi hao wamebanwa kutokana na kumarishwa kwa jeshi la nchi hiyo na misaada kutoka Tanzania na Zimbabwe.

"Vitendo vya magaidi hao hivi sasa

Na Mwandishi Wetu

vimepungua sana kutokana na kukabiliwa vilivyo na majeshi na kwamba hufanya mashambulizi ya hapa na pale," alieleza Ndugu Dauto, ambaye aliondoka jana baada ya ziara ya wiki moja nchini.

Magaidi wa Msumbiji walianza kufanya vitendo vya ugaidi mara baada ya nchi hiyo kupata uhuru 1975, lakini hivi sasa wanafyekwa na majeshi ya nchi hiyo na wengine wameanza kujisalimisha kwa serikali.

Ndugu Dauto alisema kuwa magaidi 200 tayari wamejisalimisha kwa serikali kufuatia kuanzishwa kwa sheria ya msamaha kwa wananchi wake ambao wamekuwa wakijihusi-

sha na vitendo vya ugaidi.

"Wengi wa magaidi waltojalisimisha kwa Serikali wametoka katika majimbo ya Manica, Zambezia na Sofala," alisema.

Serikali ya Msumbiji ambayo iliunda sheria ya msamaha, Desemba 1987, pia imekwishawaachia magaidi wengine 200 waliokamatwa na Serikali kutokana na vitendo vya ugaidi. alisema.

Sheria ya msamaha inawahusu tu wananchi wa Msumbiji ambao pia wamepeva mwanya wa kujisalimisha hata kwenye ofisi za ubalozi katika nchi za nje na katika ofisi za chama cha Msalaba Mwekundu.

Alipoulizwa iwapo uundaji wa sheria hiyo ni hatua mojawapo kwa serikali ya nchi hiyo kutaka kufanya mazungumzo ya mapatano, na magaidi waziri huyo alisema Msumbiji kamwe haitafanya mazungumzo na magaidi ambao aliwataja kuwa ni wauaji na wahujumu wa uchumi".

"Msumbiji kamwe haitokubali kufanya mazungumzo na magaidi wa MNR ambao ni wauaji. Mapatano yetu na magaidi wasiokubali kujisalimisha itakuwa ni kwa njia ya mapambano," alisisitiza Ndugu Dauto.

Waziri huyo hata hivyo alikiri kuwa vitendo hivyo vimesababisha hasara kubwa na vifo kwa wananchi na pia kuvuruga uchumi na huduma muhimu za jamii kama shule na hospitali.

"Kila mwaka hivi sasa karibu watoto 350,000 wanakosa kuhudhuria shule kutokana na shule nyingi kuharibiwa," alisema Ndugu Dauto.